# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

## UTABIRI WA MSIMU WA OKTOBA – DISEMBA 2017 (VULI) KWA TANZANIA






Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe : met@meteo.go.tz

**Dondoo muhimu za msimu wa mvua kipindi cha Oktoba-Disemba 2017**

Taarifa hii inatoa mwelekeo wa msimu wa mvua na uchambuzi wa mifumo ya hali ya hewa katika kipindi cha Oktoba - Disemba 2017 (Vuli) na athari zake kwa sekta mbali mbali zinazohusiana zaidi na hali ya hewa katika utekelezaji wa majukumu yake kama vile kilimo na usalama wa chakula, mifugo na wanyamapori, maliasili na utalii, nishati na maji, mamlaka za miji, afya pamoja na menejimenti za maafa. Mwelekeo wa mvua za Vuli katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2017 na athari zake unaonesha kuwa: -

Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu, Shinyanga, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Kilimanjaro, Arusha na Manyara, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja and Pemba.Utabiri wa mvua katika maeneo mengine ya nchi yaliyosalia utatolewa mwezi wa Oktoba 2017.

- Hata hivyo, mvua za chini ya wastani na vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza hususan katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Pwani, Tanga, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba.

- Pamoja na matarajio hayo ya mvua za wastani katika maeneo mengi ya nchi, uwezekano wa matukio ya vipindi vya mvua kubwa unatarajiwa hususan katika mwezi wa Disemba, 2017.

- Mtawanyiko hafifu wa mvua na vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo katika kipindi cha msimu wa mvua wa Oktoba hadi Disemba, 2017 hususan katika maeneo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Kilimanjaro, Arusha na Manyara, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja and Pemba.

- Wakulima katika maeneo hayo wanashauriwa kuandaa mashamba yao mapema na kupanda mazao yanayokomaa katika muda mfupi.

- Mamlaka husika, kama vile wadau wa Afya, menejimenti za maafa, Mamlaka za miji na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika kupunguza athari mbaya zinazoweza kutokea katika msimu wa mvua za Vuli 2017.

- Kwa ujumala maeneo mengi yaliyopo kaskazini mwa nchi yanatarajiwa kupata mvua za wastani na uwezekano wa vipindi vifupi vya mvua kubwa hususan katika mwezi wa Desemba 2017.



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :

## I. MWELEKEO WA MSIMU WA MVUA KIPINDI CHA OKTOBA – DISEMBA 2017.

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele II cha taarifa hii), kuna uwezekano mkubwa wa mvua za wastani katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, mtawanyiko hafifu wa mvua na vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo husasan katika kipindi cha miezi ya Oktoba hadi Novemba, 2017 kwa maeneo ya Nyanda za juu Kaskazini mashariki na pwani ya Kaskazini. Vipindi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza zaidi katika mwezi Disemba, 2017. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

### (i) Mvua za msimu wa 'Vuli'

Msimu wa mvua wa Oktoba hadi Disemba (vuli) ni mahususi kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (Ukanda wa Ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki, Pwani ya kaskazini na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma). Mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika maeneo ya magharibi mwa Ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini, mkoa wa Kilimanjaro na kaskazini mwa mkoa wa Kigoma; wakati katika maeneo ya mikoa ya Arusha na Manyara pamoja na maeneo ya mashariki na kusini mwa Ziwa Viktoria zinatarajiwa mvua za wastani hadi juu ya wastani .

Mvua za *Vuli, 2017* zinatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2017 katika maeneo mengi ya Ziwa Viktoria na mwezi Oktoba, 2017 katika ukanda wa pwani, na baadaye mwezi Novemba katika maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika miezi ya Novemba na Disemba, 2017 na hali kadhalika vipindi virefu vya ukavu vinatarajiwa kujitokeza zaidi katika mwezi wa Oktoba, 2017.

***Kanda ya Ziwa Victoria: (Mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Simiyu na Shinyanga):***

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuanza mapema, kati ya wiki ya pili na tatu ya mwezi Septemba, 2017 katika maeneo ya mkoa wa Kagera na kusambaa katika mikoa ya Geita, Mwanza, Mara, Simiyu na Shinyanga ifikapo wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Oktoba, 2017. Mvua hizo zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika mikoa ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga na Simiyu na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi chini ya wastani katika mkoa wa Kagera. Mvua za msimu wa Vuli zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2017 katika maeneo mengi ya Ziwa Viktoria, isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Mwanza ambapo mvua zinatarajiwa kuisha mapema katika wiki ya tatu ya mwezi Disemba, 2017.

***Ukanda wa Pwani ya Kaskazini: (Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Pwani, Visiwa vya Unguja na Pemba pamoja na maeneo ya kaskazini mwa mkoa wa Morogoro):***

Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Oktoba, 2017. Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Pwani ambayo yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Msimu wa mvua za Vuli, 2017 unatarajiwa kuwa na vipindi virefu vya ukavu katika baadhi ya maeneo hususani katika mwezi Oktoba, 2017. Mvua katika maeneo tajwa zinatarajia kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2017.

***Nyanda za juu Kaskazini Mashariki: (Kilimanjaro, Arusha na Manyara):***

Mvua zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2017 na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi ya mikoa ya Manyara na Arusha. Hata hivyo, maeneo mengi ya mkoa wa Kilimanjaro yanatarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi chini ya wastani. Mvua hizi zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Disemba, 2017.


Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :




**Picha 1 – Ramani ya wastani wa mvua – kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za mwezi Oktoba hadi Disemba; Kushoto: Mwelekeo wa mvua katika msimu huu wa Oktoba hadi Disemba, 2017.**

**Angalizo:**

***Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza yakajitokeza katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani na chini ya wastani.***

**(II) MIFUMO YA HALI YA HEWA**

Hali ya joto la juu ya wastani iliyopo magharibi mwa Bahari ya Hindi inatarajiwa kuendelea katika kipindi cha Oktoba-Disemba, 2017. Kwa upande mwingine hali ya joto la wastani inatarajiwa katikati mwa eneo la Kiikweta la Bahari ya Pasifiki. Katika kipindi cha msimu wa Vuli, 2017 hali ya joto la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Atlantiki (Pwani ya Angola).

Katika kipindi cha msimu wa Vuli, 2017 vipindi vya migandamizo midogo ya hewa vinatarajiwa kujitokeza katika eneo la pwani ya Somalia hivyo kuchelewesha kuhama kwa ukanda wa mvua kuelekea kusini mwa Ikweta. Hali hiyo, inatarajiwa kusababisha kuchelewa kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli 2017. Vimbunga vinatarajiwa kujitokeza katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hivyo kupelekea


Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :

upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka misitu ya Kongo na kuingia nchini. Hali hii ya upepo kutoka katika misitu ya Kongo inatarajiwa kusababisha vipindi vya ongezeko la mvua katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

## (III) ATHARI NA USHAURI

**Kilimo na Usalama wa Chakula, Mifugo na Wanyama pori.**

Hali ya unyevunyavu kwa ajili ya mazao na malisho ya mifugo na Wanyama pori inatarajiwa kuwa ya kuridhisha hususani katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Wakulima wanashauriwa kuandaa mashamba yao mapema na kupanda mazao yanayokomaa katika muda mfupi kwa kufuata ushauri wa wataalam wa kilimo. Wafugaji wanashauriwa kuvuna mifugo yao ikiwa katika hali nzuri kiafya na pia kuvuna maji na kuhifadhi malisho ili kukidhi mahitaji katika kipindi cha upungufu.

Upungufu wa unyevunyevu unatarajiwa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, wakulima katika maeneo haya wanashauriwa kupanda mazao yanayotumia muda mfupi kukomaa na yanayostahimili mvua chache wakifuata ushauri wa wataalam. Uzalishaji wa samaki katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani unatarajiwa kuongezeka, wakati katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani uzalishaji unatarajiwa kupungua.

**Nishati na maji:**

Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za juu ya wastani, yanatarajiwa kuwa na ongezeko la maji katika mabwawa. Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuvuna maji kwa ajili ya matumizi ya baadae. Wachimbaji madini katika migodi midogomidogo wanashauriwa kuwa makini kwani ongezeko la maji katika udongo linaweza kusababisha maporomoko ya ardhi.



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :

Hata hivyo, maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani ( Baadhi ya maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki na pwani ya kaskazini) kima cha maji katika maziwa na mabwawa kinatarajiwa kupungua, hivyo matumizi mazuri ya maji kwa ajili ya umwagiliaji, matumizi ya nyumbani na uzalishaji umeme yanashauriwa kuzingatiwa.

Matumizi ya vyanzo vya nishati mbadala ya umeme yazingatiwe ili kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza katika uzalishaji umeme kwa kutumia rasilimali maji.

**Mamlaka za miji:**

Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinatarajiwa katika msimu wa mvua, hivyo mamlaka za miji pamoja na wananchi wanashauriwa kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa mifumo na njia za kupitisha maji zinafanyakazi katika kiwango cha kutosha ili kuepusha maji kutuama na kupelekea mafuriko na uharibifu wa miundombinu pamoja na upotevu wa maisha na mali.

**Afya:**

Kutokana na uhaba wa maji salama unaotarajiwa kwa shughuli za binadamu ikiwemo usafi wananchi wanashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia milipuko ya magonjwa. Aidha, Sekta ya Afya inashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

**Menejimenti ya Maafa:**

Mamlaka za maafa na wadau wengine wanashauriwa kuchukua hatua stahiki katika utunzaji wa mazingira, matumizi mazuri ya ardhi na mipango miji na maandalizi mazuri juu ya hatua stahiki zitakazotakiwa kuchukuliwa kutokana na madhara yanayoweza kusababishwa na mvua zinazotarajiwa.



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :

**Vyombo vya habari:**

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mwenendo wa hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa ustawi wa jamii.

Mamlaka inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ujenzi, Nishati, wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.

***Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi mitatu) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo madogo utazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda mfupi na wa kati. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.***

Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.

Imetolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania:

Dkt. Agnes L. Kijazi
**Mkurugenzi Mkuu**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,S.L.P. 3056 Dar es Salaam, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Simu: 255 (0) 22 – 2460706- 8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460735; Barua pepe :